


Hii gazeti ina andikwa na shirika lisilokuwa la kiserekali Internews kwa ushirikiano na wizara ya afia na Shirikisho la Kimataifa la Msalaba Mwekunda na Jumuiya Nyekunda kwa kujibu kwenyi mahitaji za habari ya jamii.

Kila juma, tunakusanya na kuchambuwa maioni ya jamii (uvumi yani habari zenyi hazina uhakika, wasiwasi, maulizo, na kazalika) na tunatafuta majibu ku toka kwa wataalamu kwa kushirikisha jamii. Maulizo hizo zinachunguzwa kulingana na maana(umuhimu) yazo na mwendeleo wazo.

Fuateni habari za jibu juu ya Ebola katika gazeti ya Radio **"Koma Ebola"**

 [soundcloud.com/user-740750674](https://soundcloud.com/user-740750674)  
 [Facebook.com/komaebola](https://Facebook.com/komaebola)  
 [@Ebolakoma](https://Twitter.com/@Ebolakoma)  
 [koma-ebola.info](https://koma-ebola.info)



## EBOLA

### SWALI

Tunaweza sema nini juu huyu mugonjwa mwenye alikimbiaka hapa Beni na anarudiya akisema kama alisha pona?

### JIBU

Kesi ya huyu mutu ingali mu uchunguzi. Vikundi vya uongozi wa majibu (riposte) ya kupiganisha Ebola vinataka kuhakikisha kama ni kweli ni ule mutu mwenyi alikuwaka ametajwa kukuwa mugonjwa wa virusi mwenyi alikimbiaka njo mwenye alirudia.

Kama ni ule mutu, mbele ya kutangaza uponyaji wake, atapimiwa Ebola kwenye laboratoire (fasi ya vipimo). Kama matokeo ya kipimo inaonesha kama kwa kweli amepona, ataingia ndani ya kikundi kya waliopona Ebola ili afaidike na mpango ya ufuatiliaji na kupata matunzo inayo faa. Kama sivyo, ataanza fuata matunzo ya magonjwa ya Virus ya Ebola.

Lakini, inaomba kusema kama haiko njo mutu wa kwanza mwenyi anajiponea ye pekee, kama iyi kesi ilikuwa ya kweli. Utafiti (Recherche) kuhusu hii ugonjwa inaendelea siku kwa siku.

## CORONAVIRUS

### SWALI

Namna gani ya kutafautisha mutu mwenyi iko na mafua na mugonjwa wa COVID-19?

### JIBU

Magonjwa hizi mbili zinaonekana na ma halama za magongwa za kupumua za sawa sawa. Lakini, kunakuwa utafauti za sana kati ya virusi ya mafua na virusi mpya ya corona zenyi zinaweza hakikishwa tu ku laboratoire.

Zile virusi zote mbili zinaambukianaka mbio mbio kupitia kugusana ya watu na kupitia njia ya kupumua. Na kwa hiyo ni ya lazima kwa kila mutu kuheshimia hatua za kujikinga (kunawa mikono mzuri, kuvala maske saa zote, kugohola ndani ya mkunjo wa konongo yako ao ndani ya kitambala yenyi inaweza tupwa mara moja kisha kutumikishwa,...).



Fuateni habari za jibu juu ya Ebola  
katika gazeti ya Radio "Koma  
Ebola"

[soundcloud.com/user-740750674](https://soundcloud.com/user-740750674)  
[Facebook.com/komaebola](https://www.facebook.com/komaebola)  
 @Ebolakoma  
[koma-ebola.info](http://koma-ebola.info)



## EBOLA

### SWALI

Ni kweli kwamba ni sababu ya maandamano mengi ya watu wa Beni njo maana kikundi ya uongozi haitangaze tena kesi ya Ebola Beni?

### JIBU

Hapana, maandamano haiwezi zuia kikundi ya uongozi kutangaza kesi ya Ebola yenyi imehakikishwa.

Katika miripuko zote za magonjwa za Ebola, kunakuwaka kila mara maandamano, shambulio, upinzani na zaidi, kutokea ngambo ya sehemu moja ya raiya ambayo haisikie vizuri maana ya kazi za riposte. Lakini, kikundi ya uongozi kila siku inatumika kwa kupasha habari, kusikilizisha na kushurikisha jamii.

Kwa sasa Kivu ya kaskazini (Nord Kivu), habatangaze kesi ya mpya ya Ebola juu tu hakuna kesi yenyi imehakikishwa. Kama kunakuwa kesi yenyi inahakikishwa, kundi ya uongozi itafanya tangazo na itafuata hatua yote ya kawaida kwa kukinga jamii.

## CORONAVIRUS

### SWALI

2. Sababu gani kukataza ma activités na safari kat i ya Goma na Rutshuru, na japo Rutshuru hakuna ako ma kesi za mashaka ao zenyi zimehakikishwa za virusi ya corona?

### JIBU

Safari kat i ya Goma na Rutshuru zilikatazwa kwa kupunguza usambazaji wa virusi ya corona kat i ya zile maeneo mbili; sababu kat i ya ma kesi zilizo hakikishwa zenyi zilitangazwa Nord-Kivu, kulikuwa batu benye banatokea Rutshuru. Batu benyi balijongeleana nabo balijulikana na banafuutiliwa.

Hii gazeti ina andikwa kwa msaada wa watu wa Amerika kupertia Shirika ya Amerika kwa maendeleo ya kimataifa (USAID).  
Yaliyomo haionyeshi maoni ya USAID na serikali ya Amerika.



**USAID**  
FROM THE AMERICAN PEOPLE



**TRANSLATORS  
WITHOUT BORDERS**

**PAUL G. ALLEN  
FAMILY FOUNDATION**

**Internews**  
Local voices. Global change.

